

Msamaria Mwema

Hadithi ya Msamaria mwema kwenye Biblia ni mojawapo ya hadithi kuu kwenye historia. Unaweza kuisoma katika Luka 10:25-37. Mtu mmoja aliyekuwa akielekea Yeriko alivamiwa na wanyanganyi na kuachwa hali mahututi. Kwa muda saa chache zilizofuata watu watatu walimpita mtu huyu lakini ni mmoja wao tu ndiye aliyemsaidia. Mtu wa kwanza, Kuhani, aliyepaswa kujua upendo wa Mungu, alimpita tu. Wa pili, mlawi, mtu ambaye pia anafahamu sheria ya Mungu, anapita na kumpuuzua. Hatimaye, Msamaria, mtu wa nje anapita na kumsaidia mtu yule aliyeachwa hali mahututi.

Yesu alisimulia hadithi hii wakati mwanasheria alipouliza kuwa alipaswa kufanya nini ili aweze kuurithi uzima wa Milele, au kwa maneno mengine jinsi ya kufanya kumpendeza Mungu. Yesu anamwuliza mwanasheria mtazamo wake na akajibu, "Mpende Bwana Mungu wako kwa moyo wako wote na kwa nafsi yako yote na kwa nguvu zako zote na kwa nia yako yote." Na pia, "Mpende jirani yako kama unavyojipenda mwenyewe." Yesu akasema kuwa yuko sahihi ila anampa changamoto zaidi. Yesu anasimulia hadithi ya Msamaria mwema kisha anauliza, "Je, kati ya hao watu watatu unadhani ni nani aliyekuwa jirani ya mtu aliyeangukia mikononi mwa wanyanganyi?" Mwanasheria akajibu, "Yule aliyemhurumia." Kisha Yesu akamwambia aende akafanye vivyo hivyo.

Hilo ni rahisi kulifahamu sio? Kwa hakika hapana! Mwanasheria angewatambua Kuhani na Mlawi kwa heshima kuu. Angewaza kwamba Msamaria hangeweza kuwa wa msaada wowote. Wasamaria walidharauliwa kama watu wa chini wasiofuata sheria zake Mungu kikamilifu. Yesu anabadilisha matarajio ya wakili huyu juu chini kwamba yule ambaye hakutarajiwa ndiye mwenye matendo yaliyompendeza Mungu.

Kwenye vijiji vyetu tunaweza kuwapuuzua watu ambao, hatuwapendi au hatukubaliani, au wadhaifu, wagonjwa au waliodharauliwa. Hiyo sio njia ya Mungu. Anataka tuwapende na kuwakubali watu hawa kwa usawa. Jamii ya Mungu inahitaji wale wanaomjua Yesu pamoja na wale ambao wameanza kumjua, na wale ambao bado hawamjui. Watu wa 'nje' haswa wanakaribishwa. Kusudi la funzo hili nikumpendeza Mungu na twahitaji 'Wasamaria' kila upande kufanya hivi pamoja.

Kuwa wazi jinsi Mungu anavyokuunganisha na watu wengine maishani mwako. Tumia nafasi hizo kufunza kuhusu Yesu na kushirikiana na yeyote ambaye Mungu anamleta mbele zetu.

Zingatia!

Yesu anapomwambia wakili kwenda na kutenda hivyo hakika anamaanisha. Ni nani karibu nasi tunahitaji kumwonyesha upendo na kuwasaidia kwa matendo?

Pili, nani tunayemwona kama Msamaria? Ni kina nani wa nje, wale ambao hatuwezi kuwatambua kama jamii ya Mungu? Chukua muda nao, pata kuwajua na pengine kufanya kitu nao kwenye kijiji chako pamoja? kuwa wema 'Wasamaria' pamoja.


Omba:

- 1) Mungu atawajaza na huruma zake.
- 2) Mungu atatumia wale watu wasiotarajiwa kule tumaini kwenye vijiji vyetu.



Wakati Brenda alisema, "Najua mimi ni mfu aliye hai" alikuwa anazungumzia hali yake ya virusi vya ukimwi. Tangu wakati huo huo amemjua Yesu kupitia Kundi la Maisha na kutambua furaha mpya. Ameanzisha kikundi kuwasaidia wengine wanaoteseka na virusi vya Ukimwi. Anawasaidia kumjua Yesu na kutambua furaha.

- Brenda, Katima Mulilio, Namibia



Funzo hili limechochewa na "Kila Mtu ana Sehemu" funzo katika Panda, kitabu kinachowasaidia watu kupanda na kuendeleza Vikundi vya Maisha kwenye vijiji vyao. Kwa maelezo zaidi:

dignityonline.org.uk/publications